



RIPOTI YA KIHAIIDROLOJIA JARIDA LA MWEZI

BWAWA LA MTERA

Agosti, 2026



"KILA TONE LINATHAMANI"


Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00

Muhtasari wa Hali ya Maji

Bwawa la Mtera hupokea maji kutoka kwenye mito mikuu mitatu ya Great Ruaha, Little Ruaha na Kizigo, ambayo yote ipo ndani ya kidakio cha Mto Great Ruaha. Mito hii ina mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kuwezesha uzalishaji wa umeme wa maji, kusaidia shughuli za kilimo cha umwagiliaji, kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa matumizi ya majumbani, viwandani na mifugo, pamoja na kuhifadhi mtiririko wa mazingira unaohitajika kwa uhai wa mifumo ikolojia na ustawi wa maeneo yaliyopo chini ya mkondo wa mto.

Hadi kufikia mwishoni mwa Agosti 2026, mtiririko wa maji unaoingia katika Bwawa la Mtera ulikuwa sawa na asilimia 62 ya wastani wa muda mrefu (Long-Term Average – LTA) wa mwezi huo, hali inayoashiria kuwa upatikanaji wa maji ulikuwa katika kiwango cha kawaida. Hali hii ilitokana na mvua zilizonyesha kwa kiwango cha wastani katika maeneo ya juu ya kidakio, sambamba na usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji uliofanyika katika Bonde la Rufiji.

Kiwango cha maji katika Bwawa la Mtera kiliendelea kuwa juu ya wastani wa muda mrefu katika kipindi chote cha Agosti 2026. Kufikia tarehe 31 Agosti 2026, kiwango cha maji kilifikia mita 697.47 kutoka usawa wa bahari (m amsl), sawa na 100.63% ya wastani wa muda mrefu wa mwezi huo. Hali hii iliendelea kuwezesha uzalishaji wa umeme wa maji pamoja na kukidhi mahitaji mengine ya maji.



Hali ya Hewa

Hali ya Mvua – Agosti 2026:


Taarifa za mvua zinaonesha kuwa maeneo mengi ya bonde yalikuwa na hali ya ukavu katika kipindi chote cha Agosti 2026. Kutokana na hali hiyo, kulikuwa na mtiririko mdogo wa maji kutoka kwenye uso wa ardhi kwenda kwenye mito, hali iliyosababisha kupungua kwa mtiririko katika mito na vijito, hasa vile vinavyotegemea mvua za msimu.

Mwelekeo wa Hali ya Hewa – Septemba 2026:


Kwa mujibu wa utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), mvua nyepesi hadi za wastani zinatarajiwa katika maeneo mbalimbali ya Bonde la Rufiji mwezi Septemba 2026. Utabiri wa kila wiki unaonesha kuwa mtawanyiko wa mvua unaweza kutofautiana katika maeneo mbalimbali ya bonde.

Wiki ya Kwanza	Wiki ya Pili	Wiki ya Tatu	Wiki ya Nne
Mvua nyepesi hadi mvua katika maeneo ya kati na mashariki	Mvua nyepesi hadi mvua katika maeneo ya kati na mashariki	Mvua nyepesi hadi mvua katika maeneo ya kati na mashariki	Mvua nyepesi


Utabiri wa Mvua
Wiki 01 Septemba, 2026




Utabiri wa Mvua
Wiki 02 Septemba, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 03 Septemba, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 04 Septemba, 2026



Hali ya Mtiririko wa Maji

Vituo vya Kihaidrolojia



Kwa ujumla, wastani wa mtiririko wa mito katika Bonde la Great Ruaha wakati wa Agosti 2026 ulikuwa karibu na wastani wa muda mrefu, ingawa tofauti zilionekana kati ya mito mbalimbali. Jedwali 1 linaelezea mchanagnuo wa takwimu za wingi wa maji katika mito inayoingiza maji katika bwawa la Mtera.

Matokeo ya Kihidrolojia


Kwa ujumla, mito mingi ilionesha kupungua kwa mtiririko katika kipindi cha Agosti 2026 kutokana na hali ya ukavu iliyokuwepo. Hata hivyo, Mto Little Ruaha katika kituo cha Mawande uliendelea kuwa na mtiririko ulio juu kidogo ya wastani wa muda mrefu, kutokana na usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji na udhibiti wa uchoaji wa maji katika maeneo ya juu ya bonde

Jedwali 1: Mchanganuo wa Takwimu za Wingi wa Maji

Na.	Namba ya Kituo	Mto	Wastani Wingi wa Maji (m3/s) Agosti 2026	Wastani Wingi wa Maji -LTA (Agosti) 2000-2025	Maelezo
1	1KA59	Great Ruaha at Msembe	1.72	2.29	Wastani
2	1KA31	Little Ruaha at Mawande	11.74	10.69	Wastani
3	1KA42A	Kizigo at Chinugulu	0	0.64	Chini zaidi ya Wastani



Hali ya Maji Bwawani



Kufikia mwisho wa mwezi Agosti 2026:

- Hali ya usawa wa maji katika bwawa la Mtera iliendelea kuwa juu ya kiwango cha maji cha uzalishaji umeme (Maximum Operational Level)
- Kiwango cha maji katika Bwawa la Mtera kilikuwa mita 697.47 kutoka usawa wa bahari, sawa na 100.63% ya wastani wa muda mrefu wa mwezi huo.i.

Uchambuzi

- Licha ya kupungua kwa mtiririko wa maji unaoingia katika bwawa, kiwango cha maji katika Bwawa la Mtera kiliendelea kuwa juu ya wastani wa muda mrefu. Hii inaonesha kuwa uendeshaji wa bwawa pamoja na usimamizi wa rasilimali za maji ulikuwa na ufanisi katika kuhakikisha kiwango cha kutosha cha maji kinahifadhiwa.
- Hali hiyo iliwezesha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa maji, pamoja na kukidhi mahitaji ya maji kwa matumizi ya majumbani, kilimo, viwandani, mifugo na mahitaji ya kimazingira

Mapendekezo

- Kuendelea na usimamizi madhubuti wa maji na uendeshaji wa bwawa ili kuhakikisha kiwango cha kutosha cha maji kinahifadhiwa kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na mahitaji mengine ya maji.
- Kuzingatia utabiri wa mvua za El Nino unaotolewa na TMA katika kufanya maamuzi sahihi ya uendeshaji wa bwawa, usimamizi wa rasilimali za maji ili kuruhusu kiwango kitakachozidi kutolewa bila kuathiri miundombinu na wananchi waisho ukanda wa chini wa bwawa.

